

102/1

KISWAHILI (INSHA)

KARATASI YA 1

JULY/AUGUST-2015

MUDA: SAA 1¾

KAKAMEGA EVALUATION JOINT EXAM-2015

Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)

102/1

KISWAHILI (INSHA)

KARATASI YA 1

JULY/AUGUST-2015

MUDA: SAA 1¾

MAAGIZO

- Jibu jumla ya maswali **mawili**.
- Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
- Chagua swali la **pili** kutoka kwa yale **matatu** yaliyosalia.
- Kila insha isipungue maneno **400**.
- Mtihani huu una jumla ya alama **40**.

Karatasi hii ina kurasa 2 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo

1. Wewe ni katibu wa chama cha vijana cha Nishati ,mwandikie afisa wa masuala ya vijana barua ukimweleza matatizo yanayowakumba vijana katika eneo lako.

2. Pendekeza hatua zinazoweza kuchukuliwa na serikali kupambana na tatizo la gharama ya juu ya maisha nchini Kenya.
3. Andika insha inayoafiki methali , Mti mkuu ukigwa ,wana wa ndege huyumba.
4. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo,
Safari ilianza mapema Kama ilivyokuwa imepangwa,muda mchache baadaye....

Jina **Nambari yako** :.....
Sahihi
Tarehe:

102/2

KISWAHILI

Karatasi 2

Lugha

JULY/AUGUST-2015

Muda: Saa 2½

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO YA KAKAMEGA YA KATI -2015
Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)

102/2

Kiswahili

Karatasi 2

Lugha

Saa 2½

MAAGIZO

- Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulioachiwa hapo juu.
- Jibu maswali yote.
- Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SEHEMU A: UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswaliyafuatayo.

Wanawake, wanaoishi katika maeneo ya mashambani katika nchi zinazoendelea ni baadhi ya watu waliotopea na kubobea katika uchochole mkubwa. Jumla ya idadi kubwa ya wanawake hawa wanaoishi chini ya kiwango cha chini cha umaskini inakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 600. Hii ni idadi kubwa hasa ikikumbukwa kuwa ni asilimia kubwa ya wanawake wanaoishi kwenye maeneo haya.

Ulimwengu umeshuhudia ongezeko kubwa la idadi ya watu pamoja na kuwako kwa matatizo ya kiuchumi duniani. Kadhalika matatizo mengine ni mitafuruku na vita vya kikabila, majanga ya kiasili mathalani mafuriko, ukame na milipuko ya volkano. Usisahau pia kuwa kuna uharibifu wa kimazingira, mabadiliko ya desturi na kusambaratika kwa familia na misingi yake. Tatizo lingine ni kuwa kuna kuongezeka kwa hail ya wanawake kuwa wazazi pekee na hivyo kuongeza familia zinazosimamiwa na wanawake (ambao tumewataja kuwa wanakumbwa na umaskini mkubwa.)

Wanawake wanaoishi mashambani wanakumbwa na makubwa. Kwanza, kama maskini wanaishi katika mazingira magumu. Vile vile karna wanawake wanakabiliana na mapendeleo ya kisera na kitamaduni yanayowadharau na kuwapuuza wanawake na mchango wao katika maendeleo. Tatu, kama viongozi wa familia, hasa wanaolea na kutunza jamaa za mzazi mmoja, wanapambana na uongozi wa familia pamoja na uzalishaji. Aghalabu hawapati usaidizi wowote katika majukumu kama haya bali wanalazimika kupambana nayo peke yao. Kutokana na hayo yote wanawake hawapati nafasi nzuri kushiriki katika maamuzi ya maswala yanayowahusu. Maswala mengi yanaamuliwa na wanaume pasipo kuwahusisha wanawake.

Licha ya dhiki yao kubwa, wanawake hawa wanachangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa njia mbali mbali. Mchango huu unaonekana katika kiwango cha jamii, taifa na familia. Katika kiwango cha kijamii na kitaifa wanawake ndio chanzo cha nguvukazi kwani ni wao na watoto wao wanaotekeleza kazi nyingi hasa za nyumbani na mashambani. Mara nyingi huwa na uwezo bora wa kutunza chochote walicho nacho kuliko wenzao wanaume.

Kifamilia wanawake wa mashambani wanashugulika mchana kutwa katika hali ngumu ya hewa aidha jua kali au mvua huku wameeleka wanao migongoni wakilima mashamba iii kupata chakula kwa familia zao. Jukumu la kuandaa chakula nyumbani bado linaachiwa wale wale wanawake wanaokizalisha mashambani.

Jambo lisilopingika ni kwamba wanawake wanatekeleza majukumu makubwa na muhimu katika kizazi cha binadamu na ndio hasa mihimili ya jamii yoyote staarabu. Kwa hivyo, ni kinaya kitupu kudhalilisha wanawake. Mataifa mengi yaiyoendelea ni yale yaliyoondoa vikwazo vyote mbele ya wanawake na kuwaacha watekeleze wajibu wao. Kadhalika wanaume wa huko wanawaona wanawake kuwa wenzao katika kujenga jamii wala sio watumwa au watumishi wao wanaoumia na kutumikishwa kama vifaa na bidhaa. Inafaa jamii zinazodunisha wanawake zitambue kuwa ubaya wa tendo hili sio tu kudumaza

maendeleo yake bali pia kutoa mfano mbaya kwa vijana ambap wataendeleza ukandamizaji huu kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo, jamii inawajibika kutenda lilio sawa kwa kuwapa hadhi wanawake wote.

Maswali

- a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)

.....
.....

- b) Nakili maafa matatu ya kimaumbile yaliyotajwa katika kifungu hiki. (alama 3)

.....
.....

- c) Eleza sababu tatu zinazowazuia wanawake kushiriki katika maamuzi ya masuala yanayowahusu kulingana na makala haya. (alama3)

.....
.....
.....
.....

- d) Wanawake hutekeleza majukumu gani katikajamii na taifa kutokana na makala haya? (alama 3)

.....
.....
.....
.....

- e) Kuna tofauti gani baina ya wanawake wa mataifa yaliyoendelea na yale ambayo hayajastawi. (alama2)

.....
.....

- f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye taarifa. (alama 3)

(i) uchochole

.....
.....

(ii) kudhalilisha

.....
.....

(iii) mitafuruku

.....

2. MUHTASARI

Kuna fikra inayotawala siku hizi kuwajela si mahali pa adhabu bali matibabu. Yaani lengo la kumfunga mhalifu si kumuadhibu bali kumtibu kwa njia ya kurekebisha tabia iii aweze kuchangia katika maendeleo ya jamii yake anapoachiliwa.

Wataalamu wa masuala ya urekebishaji tabia wanasema kuwa mhalifu akiadhibiwa sana na kufanyishwa kazi ngumu anapokuwa kifungoni, huishia kuwa sugu zaidi kuliko alipofungwa. Kwa hivyo , wataalamu wanasisitiza umuhimu wa kutilia mkazo lengo la kumtia mtu jela kuwa ni kumjenga kitabia. Mijizi, minyang’anyi na wauaji wanapotoka gerezani kama hawakubadilishwa hurejelea tabia zao na kuhatarisha zaidi maisha ya watu wengi.

IAjabu na kinaya ni kwamba baadhi ya wahalifu nchini na kwingineko wametokea kupata faida kuu kutokana na vifungo vyao. Kuna waftungwa ambao wamewahi kuandika hadithi za kuisisimua kuhusu maisha yao na kutokea kuwa mabilionea. Magazeti na vyombo vya habari pia huvutiwa na habari kuhusu maisha yao. Mara kwa mara, magazeti hujaa habari kuhusu mambo kama haya. Pia kuna sinema nyingi ambazo zimetungwa kufuata maisha ya wahalifu fulani.

Watetezi wa haki za kibinadamu wanadai kuwa yale wafungwa walikuwa wakitendewa, na bado wanatendewa katika nchi nyingine, ni kinyume na haki za kimsingi za binadamu. Hali hii imepelekea magereza mengi kukarabatiwa iii kuweza kukidhi mahitaji ya “ubinadamu”.

Nehini Kenya, wafungwa sasa wameanza kushughulikiwa kwa kila hali. Sikwambii wanapata chakula kizuri chenye viinilishe bora, malazi bora, maji safi na mazingira nadhifu kwajumla. Kumeanzishwa pia mpango wa elimu ambao ni maalumu kwa wafungwa magerezani. Sasa wafungwa wanapata elimu na kuhudhuria madarasa na hata kuufanya mtihani wa kitaifa. Vilevile magereza nchini yameanzisha pia mpango wa kuwa na mashindano ya kila ama ya kati ya magereza mbalimbali. Kuna mashindano ya michezo mathalan kandanda, voliboli, na michezo mingine najuu ya yote, maajuzi magereza yalianzisha masliindano ya urembo baina ya wafungwa wa kike.

Kilele cha kuboreshwa kwa hali za magereza nchini Kenya ni kuanzishwa kwa huduma za kuwastarehesha wafungwa hao. Sasa wafungwa wa humu nchini wanaweza kusoma magazeti na hata kutazama runinga ili kupata habari kuhusu yanayotendeka nchini wanapoendelea kutumikia vifungo vyao.

Hata ingawa serikali imeanzisha mipango hii ya kuboresha hali katika magereza ya Kenya, kuna matatizo mbalimbali ambayo yanaendelea kukumba taasisi hii. Kwanza, ni msongamano wa wafungwa uliopo. Magereza mengi yana wafungwa maradufu ikilinganishwa na idadi yanayofaa kuwa nayo. Hali hii imepelekea kuzuka kwa magonjwa na madhara mengine. Ru imewafanya watetezi wa haki za kibinadamu

kuitaka serikali ianzishe mpango wa kutoa vifungo vya nje kwa wahalifu wenye makosa madogo madogo ili kuondoa msongamano huo.

Maswali

(a) Eleza ujumbe muhimu unaojitokeza katika aya nne za kwanza. (Maneno 40-60) alama 7, moja ya mtiririko

Matayarisho

.....
.....
.....
.....
.....
.....

Jibu

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

(b) Eleza mabadiliko ambayo yamefanywa katika idara ya magereza nchini Kenya (maneno 70-80) alama 8, moja ya mtiririkio

Matayarisho

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Jibu

.....

.....
.....
.....
.....
.....
.....

SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

a) Andika sentensi moja ukitumia kivumishi cha nomino. (alama 1)

.....

b) Eleza tofauti kati ya ama za vielezi vifuatavyo; (alama 2)

.....
.....

i) Vielezi vya namna rnfanano na;

Vielezi vya namna hali.

.....
.....

ii) Tunga sentensi mbili tofauti ukitumia vielezi vya hapo juu. (alama 2)

.....
.....

c) Tumia maneno yafuatayo katika sentensi moja ili kubainisha tofauti zao kimaana; (alama 2)

i) Chuuza

ii) Chuza

.....
.....

d) Ainisha maneno yaliyopigwa mstari. (alama 3)

i) Naam, Amekaa kabla ya Mkurugenzi Mkuu yule.

.....
.....
.....

e) landike sentensi ifuatayo upya katika hail yakinishi.

i) 1-lapo napo sipo nitakapo. (alama 1)

.....
.....

f) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao; (alama 2)

KN(N+S)+KT(T+E+E)

.....
.....
g) Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha matumizi mawili ya kinyota (*) (alama 2)

.....
.....
h) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari. (alama 3)

Uchochole wa kijinsia umepigwa marufuku na kiongozi mwenye msimamo dhabiti mnp.

.....
.....
i) Kanusha sentensi ifuatayo; (alama 2)

Angalimpata babu yangu angalimpeleka hospitalini.

.....
.....
j) Eeza maana mbili zinazopatikana katika sentensi ifuatayo; (alama 2)

Tafadhali niletee pia nichezee.

.....
.....
k) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)

“Michezo yetu ya mpira itang’oa nanga kesho,” mwalimu alimwambia mwanafunzi yule.

.....
.....
l) Akifisha sentensi ifuatayo iii ilete dhana tatu tofauti; (alama 3)

Fatuma Khamisi mjukuu wa Rashid na Rehema wameteoroka shule

.....
.....
m) i) Eleza matumizi mawili ya —po (alama 1)

.....
.....
ii) Tunga sentensi moja kubainisha matumizi hayo mawili. (alama 1)

.....
.....
n) Taja dhamira ya sentensi ifuatayo; (alama 1)

Kimbia mbio ulete sahani

.....
.....
o) Ainisha viwakilishi katika sentensi hii (alama 2)

Usibanduke papa hapa

.....
.....

p) Yakinisha sentensi hii (alama 2)

Mpishi asipokuwa mwangalifu chakula hakitaiva vizuri

.....
.....

q) Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi — nywa katika kauli ya kutendesha (alama 2)

.....
.....

r) Ukitumia njia yajedwali, changanua sentensi ifuatayo (alama 4)

Gofu hushabikiwa na watu wachache sana

.....
.....
.....
.....
.....

SEHEMU D: ISIMU JAMII

(a) Eleza juhudi zozote tano za serikali ya Kenya katika kukuza Kiswahili (alama 5)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

(b) Taja na ueleze pingamizi zozote tano zinazokwamiza juhudi za kukuza Kiswahili (alama 5)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

MTIHANI WA SHULE ZA UPILI WILAYA YA MARAKWET MAGHARIBI -2015 (MAWESSE)

Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari Nchini Kenya (K.C.S.E)

102/3

KISWAHILI

Karatasi 3

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA INSHA

UTANGULIZI

Karatasi hii imedhamiria kutathmini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi, akizingatia mada aliyopewa. Mawasiliano haya yanategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa, kwa mfano, kutunga sentensi sahihi zenye mtiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asili, ubunifu mwingi na hati nadhifu. Kwa ketegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima kutilia mkazo mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo. Mtaahiniwalazima aisome insha yote huku akizingatia sarufi, hoja, msamiati ma mtindo ili aweze kuikadhiri kwa kurejelea viwango mbalimbali vilivyo pendekekezwa. Viwango vyenyewe ni A, B, C na D kutegemea uwezo wa mtahiniwa.

VIWANGO MBALIMBALI

KIWANGO CHA D KWA JUMLA MAKI 01-05

1 Insha haieleweki kwa vyovyote vile ama uwezo wa mtahiniwa wakutumia lugha ni hafifu sana, hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile mtahiniwa anacho jaribu kuwasilisha.

2 Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa

3 Lugha imevurugika, ukafishaji na insha ina makosa ya kila aina.

4 Kujitungia swali na kulijibu

5 Insha ya urefu wa robo ikadiriwe hapa

NGAZI MBALIMBALI KIWANGO CHA D

D-(D YA CHINI) MAKI 01-02

1 Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile

2 Kujitungia swali tofauti na kulijibu

3 Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganyika ndimi.

4 Kunakili swali au maswali na kuyakariri

5 Kunakili swali au kichwa tu

D WASTANI MAKI 03

1 Mtiririko wa mawazo haupo

2 Mtahiniwa amepotoka kimaudhui.

3 Matumizi ya lugha ni hafifu mno

4 Kuna makosa mengi ya kila aina

D+ (D YA JUU) MAKI 04-05

1 Insha ya aina hii huwa na makosa mengi ya kila aina. Lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha

2 Hoja hazikukuelezwa kikamilifu / mada haikukuzwa ilivyo.

3 Mtahiniwa hana uhakika wa matumizi ya lugha.

4 Mtahiniwa hujirudiarudia

5 Insha yenyewe urefu wa nusu ikadiriwe hapa.

KIWANGO CHA C KWA JUMLA MAKI 06-10

1. Mtahiniwa anajaribu kuishughulikia mada japo hakuikuza na kuiendeleza vilivyo.

2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia / hana ubunifu wa kutosha.

3. Mtahiniwa anaakifisha sentensi vibaya.

4. Mtiririko wa mawazo unanza kujitokeza japo kwa njia hafifu.
5. Insha ina makosa mengi ya sarufi, ya nisamiati na ya tahajia (hijai.)
6. Insha yenye urefu wa nusu ikadiriwe hapa.

NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA C

C- (C YA CHINI) MAKI 06-07 .

1. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha na kutiririsha mawazo yake.
2. Mtahiniwa hana msamiati wa kutosha wala miniundo ya sentensi ifaayo.
3. Mtahiniwa ana fanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msamiati na insha yake haieleweki kwa urahisi.

C WASTANI MAKI 08

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu,
2. Dhana tofautitofauti hazijitokezi wazi.
3. Mtahiniwa hana ubunifu wa kutosha.
4. Mtiririko wa mawazo ni hafifu na hana-ufundi wa lugha unaofaa.
5. Amejaribu kuishughulikia mada aliyopewa
6. Mtahiniwa ana shida ya ukifishaji.
7. Mtahiniwa *anafanya* makosa mengi ya sarufi ya hijai na ya msamiati lakini bado insha inaeleweka. .

C+ (CYAJUU) MAKI 09-10

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri akizingatia mada lakini kwa njia isiyona mvuto.
2. Dhana tofautitofauti zinajitokeza japo kwa njia hafifu.
3. Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
4. Misenio na methali zimetumika kwa njia hafifu.
5. Ana shida ya ukifishaji.
6. Kuna makosa ya sarufi, ya msamiati na ya hijai yahayoathiri mtiririko wa mawazo.

KIWANGO CHA B KWA JUMLA MAKI 11-15

1. Katika kiwango hiki, mtahiniwa anaonyesha hali ya kuimudu lugha.
2. Mtahiniwa anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri.
3. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha.
4. Mada imekuzwa na kuudelezwa kikamilifu.
5. Insha ya urefu wa robo tatu ikadiriwe katika kiwango hiki.

NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA B

B-(B YA CHINI) MAKI 11-12 -

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri kwa kueleza hoja tofautitofauti akizingatia mada.
2. Mtahiniwa ana mtiririko mzuri wa mawazo.
3. Mtahiniwa anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia.
4. Makosa yanadhithirika/kiasi

B WASTANI MAKI 13

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha
2. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika akizingatia mada.
3. Mtahiniwa anateua na kutumia mifano michache ya msamiati mwafaka.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Makosa ni machache/kuna makosa machache.

B+ (B YA JUU) MAKI 14-15

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika na anajieleza waziwazi.
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi akizingatia mada.
3. Mtahiniwa ana mchanganyiko mzuri wa msamiati miaovuti unaovutia.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Ukifishaji wa sentensi zake ni mzuri.
6. Makosa ni machache ya hapa na pale.

KIWANGO CHA A KWA JUMLA MAKE 16-20

1. Mtahiniwa ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka akizingatia mada.
2. Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato.
3. Ana uwezo wa kutumia tamathali za usemii ili kutoa hisia zake kwa njia bora na kwa urahisi.
4. Umbuji wake unadhihirisha ukomavu na ukakamavu wake kimawazo.
5. Insha ina urefu kamili.

NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA A

A- (YA CHINT) MAKI 16-17

1. Mtahiniwa anadhihirisha ukomavu wa lugha.
2. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika na anashughulikia mada.
3. Ana mtiririko mzuri wa mawazo
4. Msamiati wake ni mzuri na unaovutia.
5. Sarufi yake ni nzuri.
6. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
7. Makosa ni machache yasiyokusudiwa.

A WASTAN MAKI 18

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri kulingana na mada.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato/kunasa.
3. Anatoa hojazilizokomaa.
4. Anatumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia zaidi.
5. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
6. Makosa ni nadra kupatikana.

A+(AYAJUU) MAKI 19 - 20

1. Mawazo yanadhihirika zaidi na mada imeshughulikiwa vilivyo.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato.
3. Hoja zake zimekomaa. na zinashawishi.
4. Msamiati wake ni wa hali ya juu na unaovutia zaidi
5. Sarufi yake ni nzuri zaidi/kabisa.
6. Anatumia ntiundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
7. Makosa yote kwa jumla hayazidi matano.

VIWANGO MBALIMBALI KWA MUHTASARI

KIWANGO	NGAZI	MAKI
A	A+	19 -20
	A	18
	A-	16 - 17
B	B+	14 – 15
	B	13
	B-	11 - 12
C	C+	09 – 10
	C	08
	C-	06 - 07
D	D+	04 – 05
	D	03
	D-	01 - 02

USAHISHAJI NA UTUZAJI KWA JUMLA

Mtahini ni sharti aisome insha yote akizingatia vipengee muhimu. Vipengee hivi ni maudhui, msamiati, mtindo, sarufi na hijai.

MADHUI

1. Maudhui ni hoja au mambo yanayozungumziwa, kuelezewa au kuhadithiwa kwa mujibu wa mada iliyoteuliwa.
2. Maudhui ndio hasa uti wa mgongo wa insha yoyote ile.

3. Ubunifu wa mtahiniwa hukisiwa kwa kutathmini uzito wa maudhui yake kulingana na mada teule.

MSAMIATI

Msamiati ni jumla ya maneno yatumiwayo katika lugha husika, Mtahiniwa anatarajiwa kutumia msamiati unaooana na mada teule. Kutegemea ukwasi wa lugha alionao, mtahiniwa anatarajiwa kuikuza mada kwa kuifinyanga lugha kiufundi. Ni muhimu kuelewa kwamba kutokana na maendeleo na ukuaji wa teknolojia na mawasiliano, maneno mapya yanaibuka kila uchao.

MTINDO

Mtindo unahusu mambo yafuatayo.

- Mpangilio wa kazi kiaya.
- Mtiririko na mshikamano wa mawazo kiaya na katika insha nzima.
- Hati nzuri na inayosomeka kwa urahisi.
- Matumizi ya tamathali za userni, kwa mfano, methafi, misemo, jazanda na kadhalika.
- Kuandika herufi vizuri kwa mfano Jj, Pp. Uu, Ww na kadhalika.
- Sura ya insha.
- Unadhifu wa kazi ya mtahiniwa.

SARUFI

Sarufi ndio msingi wa lugha. Ufanisiwa mawasiliano hutegemea uwezo wa mtahiniwa wa kutunga sentensi sahihi zenye uwiano wa kisarufi. Mtahini ataonyesha makosa yote ya sarufi yake katika insha anayosahihisha. Makosa ya sarufi huweza kutokea katika:

- (i) Matumizi ya alama za uakifishaji.
 - (ii) Kutumia herufi kubwa au ndogo mahali pasipofaa.
 - (iii) Matumizi yasiyofaa ya ngeli na viambishi, viunganishi, nyakati, hali, vihusiano na kadhalika.
 - (iv) Mpangilio wa maneno katika sentensi.
 - (v) Mnyarbuliko wa vitenzi na majina.
 - (vi) Kuacha neno linalohitajika au kuongeza neno lisiohitajika katika sentensi.
 - (vii) Matumizi ya herufi kubwa:
a, Mwanzo wa sentensi
- (c) siku za juma, mwezi n.k.

b, Majina ya pekee.

i) Majina ya mahali, mji, nchi, mataifa na kadhalika.

ii) Mashirika, masomo, vitabu n.k.

iii) makabila, lugha nk.

vi) Jina la Mungu.

v) Majina ya kutambulisha hasa wanyama wa kufugwa, kwa mfano yale ya mbwa- F popi, simba, Tomi na menineyo

vi) majina ya watu (binadamu)

MAKOS YA HIJAI/TAHAJIA

Haya ni makosa ya maendelezo. Mtahini anashauriwa asahihishe huku akiyaonyesha yanapotokea kwa mara ya kwanza tu. Makosa ya tahajia huweza kutokea katika:

(a) Kuteaganisha neno kwa mfano 'aliye kuwa'

(b) Kuunganisha maneno kwa mfano 'kwasababu'.

(c) Kukata silabi visivyo afikapo pambizoni kama vile 'ngan – o'

(d) Kuandika herufi isiyofaa kwa mfano 'ongesa' badala ya 'ongeza'

(a) Kuacha herufi katika neno kwa mfano 'alieuja' badala ya 'aliyekuja'.

(f) Kuongeza herufi isiyohitajika kama vile 'piya' badala ya 'pia'.

(g) Kuacha alama inayotarajiwa katika herufi kama vile j i.

(11) Kukosa kuandika kistari cha kuendeleza neno afikiapo pambizoni au kukiandika mahali pasipofaa.

(i). Kuacha ritifa au kuiandika mahali pasipofaa, kwa mfano ngombe,

ngom'be, n'gombe, ng'mbe.n.k

(j) Kuandika maneno kwa kifupi kama vile k.v., k.m., .y.v., n.k. na kadhalika.

(k) Kuandika tarakimu kwa mfano 27-08-2010.

ALAMA ZA KUSAHIHISHIA

===== Hupigwa chini ya sehemu ambapo kosa la sarafi limetokea kwa mara ya kwanza tu .

----- Hupigwa chini ya seheniu au neno ambapo kjiisa la hijai imetokea kwa mara ya kwanza tu.

✓ Hutumiwa kuonyesha hoja inapokamilikia pambazoni kushoto.

λ Hutumiwa kuonyesha kuachwa kwa neno/maneno.

✓ Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutumiwa juu ya neno lenyewe.

X Hutumiwa kuonyesha msamiati usiofaa. Alama hii hutumiwa juu ya neno lenyewe.

Maelezo mafupi yanahitajika kuhusu tuzo lililotolewa. Kila ukurasa uwe na alama ya katikati ili kuthibitisha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo.

UKADIRIAJI WA UREFU WA INSHA

Maneno 9 katika kila msitari	1 ½ ukurasa mmoja na nusu.
Maneno 8 katika kila msitari	1 ¾ ukurasa mmoja na robo tatu
Maneno 7 katika kila msitari .	2 kurasa mbili
Maneno 6 katika kila msitari	2 ¼ kurasa mbili na robo
Maneno 5 katika kila msitari	2 ¾ kurasa mbili na robo tatu.
Maneno 4 katika kila msitari	3 ¾ kurasa tatu na robo tatu.
Maneno 3 katika kila msitari	4 ½ kurasa nne na nusu.

Kufikia maneno	174	Insha robo
Maneno	175- 274	Insha nusu
Maneno	275 – 374	Insha robo tatu
Maneno	375 na kuendelea	Insha kamili